

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: +255 26 2321607
Nukushi: +255 26 2322116
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**KUKANUSHA TAARIFA ILIYOTOLEWA NA MGOMBEA URAIS WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA KUPITIA CHAMA CHA DEMOKRASIA NA
MAENDELEO (CHADEMA) NDUGU TUNDU ANTIPHAS LISSU**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais -TAMISEMI) imesikitishwa na taarifa zilizotolewa hivi karibuni kupitia mitandao ya kijamii ikimuonesha mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ndugu Tundu Antiphas Lissu, akituhumu kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini wameitwa Dodoma na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, ili wapewe maelekezo maalum kuhusu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.


Tunapenda kuutarifu umma kwamba taarifa hiyo iliyotolewa na Mgombea Urais huyo akiwa Mjini Musoma ni taarifa ya uongo ambayo wananchi wote wanapaswa kuipuuza. Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ndiyo Ofisi inayowasimamia Wakurugenzi wote wa Halmashauri kwa upande wa Tanzania Bara imesikitishwa sana na taarifa hiyo ya uongo ambayo imetolewa na mtu anayeomba kupewa dhamana ya uongozi wa nchi.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inathibitisha kwamba hakuna Mkurugenzi yeyote wa Halmashauri aliyeitwa Dodoma kukutana na MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakurugenzi wote wa Halmashauri wapo katika vituo vyao vya kazi wakiendelea kutimiza wajibu wao wa kusimamia shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma kwa wananchi katika Halmashauri zao pamoja na kusimamia maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa kuzingatia miongozo mbalimbali kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Wananchi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini ndio mashahidi wanaoshuhudia Wakurugenzi wao wa Halmashauri wakiwa katika maeneo yao wakitimiza majukumu yao. Taarifa hiyo inaonesha wazi kwamba mtoa taarifa alikuwa na nia ovi kwa umma ili kupotosha ukweli na kuwakatisha tamaa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ni Wasimamizi wa Uchaguzi kwa nia ya kuvuruga Uchaguzi Mkuu na kuharibu amani ya nchi kwa makusudi.

Hivyo, Ofisi ya Rais -TAMISEMI inawaomba **Watanzania wote waipuuze taarifa hiyo ya uongo** sambamba na kuwaomba Viongozi wa Dini zote nchini na wananchi wote kuendelea kuliombea Taifa letu wakati huu tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu ili yeyote mwenye nia mbaya ya kutaka kuvuruga amani ya nchi yetu kwa makusudi asiweze kufanikiwa.

Imetolewa na:


Eng. Joseph M. Nyamhanga.
KATIBU MKUU
Ofisi ya Rais - TAMISEMI